MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

TAARIFA KWA UMMA JUU YA KUFUTIA USAJILI VYUO VILIVYOKIUKA TARATIBU ZA USAJILI ZA VETA

UTANGULIZI

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ni chombo cha umma kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 1 ya mwaka 1994 [na kufanyiwa marekebisho mwaka 2006] kwa ajili ya kuratibu, kudhibiti ubora, kuendeleza, na kugharamia elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

Usajili na Utoaji Ithibati kwa vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini ni miongoni mwa wajibu wa VETA katika kutekeleza jukumu la kuthibiti ubora wa mafunzo ya Ufundi stadi. Vyuo vyote vinavyotoa mafunzo ya ufundi stadi nchini, vikiwemo vinavyomilikiwa na watu binafsi, taasisi binafsi, au umma vinapaswa kusajiliwa na kupata ithibati kutoka VETA kabla ya kuanza kutoa mafunzo.

VIGEZO VINAVYOTUMIKA KUSAJILI

Vigezo vinavyotumika kusajili vyuo vinavyotoa elimu na mafunzo ya ufundi stadi ni kama vifuatavyo:

1. **Mitaala:** Chuo kinapaswa kutumia mitaala iliyoidhinishwa na Bodi inayosimamia Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

2. **Watumishi (Walimu na wasio walimu):** Chuo kinapaswa kuwa na watumishi wa kutosha na wenye viwango vya elimu vinavyowiana na matakwa ya majukumu ya nafasi zao za kazi kama ilivyoanishwa katika miongozo ya kuanzisha vyuo;

3. **Zana na nyenzo za kufundishia:** Chuo kinapaswa kuwa na zana na nyenzo za kutosha kufundishia fani husika kama ilivyoainishwa katika miongozo;

4. **Miundombinu:** Chuo hupaswa kuwa na miundombinu na mazingira yanayofaa na kukidhi vigezo vya utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi kama ilivyoainishwa katika miongozo;

5. **Vyanzo vya fedha:** Chuo hupaswa kuthibitisha kuwa kina vyanzo vya fedha vya kutosha na endelevu kwa ajili ya kutoa elimu na mafunzo yanayotarajiwa; na

6. **Huduma muhimu:** Chuo hupaswa pia kuwa na huduma muhimu zikiwemo maji, umeme, mawasiliano, na usafiri.

VIGEZO VINAVYOTUMIKA KUTOA ITHIBATI

Vigezo vya kutoa ithibati kwa vyuo ni pamoja na:

1. Mafunzo pendekezwa kuwa na mantiki na yenye kuhitajika kwenye soko la ajira;
2. Kuwa na miundo mbinu inayowezesha kutoa mafunzo kwa ufasaha na ufanisi;
3. Kuwa na zana na nyenzo bora za kufundishia; na
4. Kuwa na vifaa vya mawasiliano vinavyosaidia kutoa mafunzo.
5. Kuwa na walimu wenye viwango vya elimu vinavyostahili kufundisha mafunzo husika;
6. Kuwa na wanafunzi wenye uwezo wa kufuatilia mafunzo kulingana na mitaala husika;
7. Kuwa na mfumo mzuri wa usimamizi wa mafunzo;
8. Kuwa na mifumo ya ndani ya kudhibiti ubora (internal quality assurance) wa mafunzo;
9. Kuwa na utamaduni unaofaa wa uadilifu na uaminifu; na
10. Uwezo wa kifedha na kukubalika kwa mafunzo kwenye soko la ajira pamoja na utawala bora wa chuo unaoshirikisha wadau.

MADARAJA YA USAJILI

Usajili hufanyika katika Madaraja manne yaani daraja A, B, C na D. Vyeti vya usajili huonyesha daraja la usajili na fani zinazoruhusiwa kutolewa katika chuo kulingana na uwezo wake. Madaraja hayo na sifa zake ni kama ifuatavyo:

CATEGORY A	CATEGORY B	CATEGORY C	CATEGORY D
Chuo chenye uwezo wa kutoa mafunzo kuanzia fani 8 kutoka sekta tofauti au zaidi na fani 4 kutoka sekta moja. Angalau fani 4 kutoa zaidi ya ngazi ya pili (level II)	Chuo chenye uwezo wa kutoa kuanzia fani 5 toka kwenye sekta tofauti na fani 2 katika sekta moja. Angalau fani mbili kutolewa mpaka ngazi ya pili (level II)	Chuo chenye uwezo wa kutoa kuanzia fani moja kuanzia kufikia ngazi ya pili (Level II).	Chuo chenye uwezo wa kutoa mafunzo kuanzia moduli moja hadi kufikia ngazi ya kwanza ya mafunzo (Level I).

Kwa hivyo, kwa mamlaka iliyonayo na kwa kuzingatia vigezo vya usajili na ithibati, VETA inautaaarifu umma kuwa vyuo vifuatavyo vimefutiwa usajili wa kutoa mafunzo ya ufundi stadi kutokana na kukiuka au kushindwa kutimiza vigezo na taratibu mbalimbali zinazotakiwa:

Na.	Jina la Chuo	Namba ya Usajili	Sababu za Kufuta Usajili	Maagizo ya Hatua za Kuchukua
1.	**Starcom Hotel Academy - IRINGA**	**VET/IRA/PR/2012/C/030**	Kubadilisha eneo la kutolea mafunzo kutoka Kilolo kwenda eneo lingine la Iringa mjini ambalo halijaidhinishwa na VETA	Chuo kiombe upya usajili katika eneo jipya na kwa kuzingatia vigezo.
2.	**Southern College of Tanzania-IRINGA**	**VET/IRA/PR/2013/D/036**	Kubadilisha eneo la kutolea mafunzo	Chuo kiombe upya usajili katika eneo jipya na kwa kuzingatia vigezo
3.	**Green House Technology VTC - DODOMA**	**VET/DOM/PR/2012/D/013**	Mmiliki alifunga kituo bila ya kuiariBu ofisi ya VETA Kanda	Kurejesha cheti cha usajili kwenye ofisi ya VETA ya Kanda
4.	**Amani VTC DODOMA**	**VET/DOM/PR/2012/C/005**	Kubadilisha chuo kuwa shule ya sekondari	Kurejesha cheti cha usajili kwenye ofisi ya VETA ya Kanda
5.	**Mikukuyumbu VTC - MTWARA**	**VET/MTR/PR/2012/D/007**	Kubadilisha chuo kuwa shule ya sekondari	Mmiliki anatakiwa kurejesha cheti cha usajili kwenye ofisi ya VETA ya Kanda
6.	**Mnero VTC- LINDI**	**VET/LND/PR/2012/C/009**	Upungufu wa zana na vifaa vya kufundishia pamoja na miundombinu kuwa chini ya kiwango	Kurejesha cheti cha usajili kwenye ofisi ya VETA ya Kanda
7.	**Majority VTC - MBEYA**	**VET/MBY/PR/2014/D/030**	Kituo kilifungwa kutokana na mgogoro wa wamiliki	Kurejesha cheti cha usajili kwenye ofisi ya VETA ya Kanda
8.	**Baraka VTC DAR ES SALAAM**	**VET/DSM/PR/2012/D/003**	Kubadilisha eneo la kutolea mafunzo kutoka Kinondoni Mkwajuni kwenda kwenye eneo lingine.	Chuo kiombe upya usajili katika eneo jipya na kuzingatia vigezo
9.	**Pure Academic of Aesthetics - DAR ES SALAAM**	**VET/DSM/PR/2012/C/042**	Kukosa wanafunzi kutokana na kutoza ada kubwa mno. Chuo kilikuwa kinatoza ada kubwa na kwa Dola za Kimarekani	Kurejesha cheti cha usajili kwenye ofisi ya VETA ya Kanda
10.	**Lamoon College of Business - DAR ES SALAAM**	**VET/DSM/PR/2013/C/053**	Kukosa Fedha Za Kuendesha Chuo. Matumizi mabaya ya fedha yaliyosababisha uhaba mkubwa wa fedha za kuendeshea mafunzo	Kurejesha cheti cha usajili kwenye ofisi ya VETA ya Kanda
11.	**Mpera VTC - SHINYANGA**	**VET/SHY/PR/2012/C/005**	Kutozingatia vigezo vya usajili	Kurejesha cheti cha usajili kwenye ofisi ya VETA ya Kanda

WAMILIKI WOTE WA VYUO VYA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NCHINI WANAKUMBUSHWA KUZINGATIA VIGEZO, MASHARTI NA TARATIBU ZOTE ZA UTOAJI MAFUNZO NA UENDESHAJI WA VYUO KAMA ZILIVYOAINISHWA KATIKA MIONGOZI MBALIMBALI INAYOTOLEWA NA VETA. VETA HAITASITA KUCHUKUA HATUA STAHIKI KWA CHUO CHOCHOTE KITAKACHOENDELEA KUKIUKA MASHARTI NA TARATIBU ZA KUTOA MAFUNZO YA UFUNDI STADI.

LENGO LA HATUA HIZI NI KUHAKIKISHA KUWA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI YANATOLEWA KOTE NCHINI NI UBORA NA YANAZALISHA WAHITIMU WENYE STADI MAHIRI.

AIDHA WAZAZI NA WADAU WOTE WANAOMBWA KUWASILIANA NA OFISI ZETU ZA KANDA KATIKA MIKOA ILIYOORODHESHWA KWENYE JEDWARI ILI KUPATA TAARIFA ZA VYUO VYA UFUNDI STADI KABLA YA KUPELEKA VIJANA WAO KUSOMA.

KANDA YA DSM (D'SALAAM) P.O.BOX 40274, DSM **Regional Director:** Habib Bukko 0784 584365 habib.bukko@yahoo.com hbukko@veta.go.tz	**KANDA YA MASHARIKI (MOROGORO)** P.O.BOX 1955, Morogoro **Regional Director:** Asanterabi M Kanza 0715 482952 akanza@veta.go.tz kanzaamani@yahoo.com vetaeasternzone@veta.go.tz
KANDA YA ZIWA – (MWANZA) P.O.BOX 1983, Mwanza **Regional Director:** Hildegardis Bitegera 0754 384563 hbitegera@veta.go.tz bestbitegera@yahoo.co.uk vetawesternzone@veta.go.tz	**KANDA YA KATI (DODOMA)** **P.O.BOX 2084, Dodoma** **Regional Director:** Ramadhani Mataka 0784 365827 rmataka@veta.go.tz
KANDA YA KUSINI MAGHARIBI (MBEYA) **P.O.BOX 2498, Mbeya** **Regional Director:** Justine Rutta 0784 263300 justine_rutta@yahoo.co.uk jrutta@veta.go.tz swz@veta.go.tz	**KANDA YA MAGHARIBI (TABORA)** P.O.BOX 1218, Tabora **Regional Director:** Wilhard Soko 0754 429294 w_soko81@yahoo.com wsoko@veta.go.tz
KANDA NYANDA ZA JUU (IRINGA) P.O.BOX 818, Iringa **Regional Director:** Suzana Magani	**KANDA YA KUSINI MAGHARIBI (MTWARA)** P.O.BOX 700, Mtwara **Regional Director:**

0784 358782 smagani@veta.go.tz susanmagani@yahoo.com	Kibehele Joseph 0713 232264 jkibehele@yahoo.com jkibehele@veta.go.tz
KANDA YA KASKAZINI (MOSHI) P.O.BOX 1738, Moshi **Regional Director:** Angelus Ngonyani 0773 150540 anmejac@yahoo.com angonyani@veta.go.tz	Kwa taarifa zaidi wasiliana na: **MKURUGENZI MKUU** VETA Makao Makuu S.L.P. 2849, Dar es Salaam Simu: 022 2863407/9 Baruapepe: info@veta.go.tz Tovuti: www.veta.go.tz

Tangazo hili linapatikana kwenye tovuti ya VETA www.veta.go.tz

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:

MKURUGENZI MKUU
VETA Makao Makuu
S.L.P. 2849, Dar es Salaam
Simu: 022 2863407/9
Baruapepe: info@veta.go.tz
Tovuti: www.veta.go.tz